



SWAHILI A1 – STANDARD LEVEL – PAPER 2
SOUAHLÉLI A1 – NIVEAU MOYEN – ÉPREUVE 2
SUAHILI A1 – NIVEL MEDIO – PRUEBA 2

Tuesday 23 May 2006 (afternoon)

Mardi 23 mai 2006 (après-midi)

Martes 23 de mayo de 2006 (tarde)

1 hour 30 minutes / 1 heure 30 minutes / 1 hora 30 minutos

INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Answer one essay question only. You must base your answer on at least two of the Part 3 works you have studied. You may include in your answer a discussion of a Part 2 work of the same genre if relevant. Answers which are not based on a discussion of at least two Part 3 works will not score high marks.

INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N'ouvrez pas cette épreuve avant d'y être autorisé(e).
- Traitez un seul sujet de composition. Vous devez baser votre réponse sur au moins deux des œuvres de la 3^e partie que vous avez étudiées. Le cas échéant, vous pouvez inclure dans votre réponse une discussion sur une œuvre du même genre littéraire étudiée dans la 2^e partie du programme. Les réponses qui ne sont pas basées sur au moins deux des œuvres de la 3^e partie n'obtiendront pas une note élevée.

INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Elija un tema de redacción. Su respuesta deberá basarse en al menos dos de las obras estudiadas en la Parte 3. Se podrán hacer comentarios sobre una obra de la Parte 2 del mismo género, si fuera necesario. Las respuestas que no incluyan una discusión sobre al menos dos obras de la Parte 3 no recibirán notas altas.

*Jibu suala moja tu la insha. Jibu lako liegemee kwenye angalau kazi mbili za kazi za sehemu ya 3 ulizojifunza. Unaweza kuingiza katika jibu lako majadiliano ya kazi ya sehemu ya 2 ya utanze huohuo ambaa umejitayarisha nao. Majibu ambayo **hayana** mjadala wa angalau kazi mbili za sehemu ya 3 **hayatapewa** alama nyngi.*

Tamthilia

1. Ama

- (a) Kwa kuzingatia kazi ulizosoma, linganisha na kutofautisha vile waandishi wa tamthilia wanavyotumia mitindo mbalimbali kuendeleza na kupitisha ujumbe wao.

Au

- (b) Maudhui ya maadili katika Jamii yamepewa nafasi muhimu katika tamthilia za kiswahili. Dhibitisha ukweli wa kauli hii ukizingatia tamthilia mbili ulizosoma na ulinganishe jinsi waandishi wanavyoshawishi na kutekeleza maudhui ya maadili.

Riwaya

2. Ama

- (a) Mitindo ya taharuki na mbinu rejeshi huwa nyenzo muhimu katika kuendeleza riwaya. Kwa kurejelea angalau riwaya mbili ulizozingatia jadili jinsi waandishi walivyotumia mbinu hizi mbili ili kuboresha uandishi wao.

Au

- (b) Ndoa na mapenzi ni vipengle muhimu za kimaisha katika jamii. Kwa kuzingatia kazi zozote mbili ulizozisoma jadili jinsi maudhui haya yalivyoendelezwa.

Ushairi

3. Ama

- (a) Matumizi ya taswira, jazanda, nahau na tashbihi ni nguzo muhimu katika ushairi. Kulingana na kazi ulizozisoma linganisha na kujadili njia tofauti ambazo mbinu hizi zimetumiwa katika ushairi.

Au

- (b) Mashairi hutungwa ili kuliwaza, kusifu na kutoa mwongozo wa kimaisha. Jadili kauli hii huku ukizingatia ni kwa kiwango kipi mitindo mbalimbali inavyochangia kuendeleza kikamilifu jukumu la ushairi.

Riwaya ya mapenzi

4. Ama

- (a) Vijana wa siku hizi hawatofautishi mapenzi ya dhati na hisia za kimwili. Ukifafanua jinsi mapenzi haya yanavyoendelezwa kwa riwaya mbili ulizosoma, jadili huku ukitoa mifano mwafaka kutoka kwenye vitabu ulivyosoma, kama kauli hii imeimarishwa au kukataliwa.

Au

- (b) Kwa kuzingatia riwaya ulizosoma, onyesha vile watu mbalimbali katika tajriba zao za kimapenzi, wanavyoteseka kutokana na kufungwa kwenye minyororo ya sheria za kimaisha zilizowekwa na jamii na ujadili kuhusu migogoro hii inavyoelezewa au kutatuliwa.

Maswali ya kijumla

5. Ama

- (a) Kwa kuzingatia kazi ulizosoma, jadili huku ukitoa mifano mwafaka mtazamo wa waandishi kuhusu swala la ubinafsi na tamaa. Onyesha vile waandishi wanavyofaulu au kushindwa kutoa suluhisho la maswala haya.

Au

- (b) Linganisha na tofautisha kazi zozote mbili ulizojitayarishia katika vipengele vyta uumbaji wa wahusika.

Au

- (c) Kwa kuzingatia kazi ulizosoma, jadili jinsi matumizi ya lugha yanavyofanikisha kupitisha au kupotosha ujumbe wa mwandishi.

Au

- (d) Fasihi inasaidia kivipi katika kuangazia matatizo mbalimbali yanayokumba jamii? Jadili kauli hii ukizingatia kazi mbili ulizozisoma.